# 'Rushwa bado kikwazo cha uwekezaji nchini'

Na Joseph Mwendapole

MAZINGIRA ya uwekezaji Tanzania yameendelea kuwa magumu kulinganisha na nchi mbalimbali duniani. Hali hiyo imeelezwa kuwa inachangiwa na vitendo vya rushwa.

Kampuni ya Best- AC ilifanya utafiti unaoonyesha kuwa mambo yanayoleta ugumu katika kuendesha biashara na kuzifanya zisikue kama inavyotakiwa ni pamoja na umeme, barabara, rushwa na maji.

Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti huo, umeme umekuwa ni tatizo la mara kwa mara na barabara zikishika nafasi ya pili, rushwa ambayo ilionekana kupungua mwaka 2010, imerudi tena na kuwa ni tatizo kubwa.

Ripoti ilisema kuwa tatizo la umeme kwa mwaka 2010, lilikuwa kubwa kiasi cha baadhi ya wenye viwanda kupunguza idadi kubwa ya wafanyakazi na kupunguza uzalishaji.

Ilisema kutokana na tatizo hilo la umeme ajira mpya zilisimama, uzalishaji ulipungua kwa kiwango kikubwa sana na uwekezaji mpya haukuwa kwa kiwango kinachotakiwa kutokana na woga wa wawekezaji kuhusu umeme.

Ilisema wawekezaji walilazimika kujichimbia visima vya maji ili waweze kuendesha shughuli zao kwa ufanisi badala ya kutegemea maji ya serikali ambayo upatikanaji wake ni wa nadra sana.

"Utafiti huo umeangalia mitizamo iwapo serikali inafanya jitihada yoyote katika kushughulikia kila moja ya vipengele hivyo . Na ugumu unaosababishwa na kila kipengele na mitizamo juu ya kiwango cha jitihada zinazofanywa na serikali kushughulikia tatizo na kisha kuhusishwa na umuhimu wake kwa mazingira kwenye orodha," ilisema sehemu ya ripoti hiyo. Hiyo ni ripoti ya nne ya mwaka juu ya viongozi wa biashara nchini Tanzania inatoa muhtasari wa mawazo yao juu ya mazingira wezeshi na nafasi ya serikali katika kuhakikisha biashara zinafanywa kwa urahisi.

Ripoti hiyo imeandaliwa ili kutoa vidokezo juu ya masuala ya vipaumbele vya kuchukuliwa hatua kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanyia biashara Tanzania.

Kazi hiyo ya utafiti iligharimiwa na Best-AC, taasisi ambayo kazi yake ni kuzisaidia taasisi za sekta binafsi (PSOs) kujihusisha katika mazungumzo kati ya sekta binafsi na za umma kwa lengo la kushawishi kuleta mabadiliko kwenye sera za umma zenye lengo la kuboresha mazingira ya biashara Tanzania.

Benki ya Dunia inaeleza kuwa kwa kuboresha mazingira wezeshi ya biashara, itasaidia kuongeza kiwango cha uwekezaji kwenye sekta binafsi, hali itakayomaanisha ni utajiri mwingi zaidi na ongezeko la ajira na kwa maana hiyo, itasaidia kupunguza umaskini.





| COMPANIES NAMES | EXPORT PRODUCTS | WEB SITE |
|---|---|---|
| ZM KABLO | Fire Resistant / Halogen-free Flame Retardant Cables, Instrumentation Cables, Control Cables Fire Alarm Cables, BUS Cables, Audio Cables, Video Cables, Coaxial & HD Cables, Computer System Cables, Close Circuit Camera System Ca, Data Transmission Cables, PUR Cables Marine and Shipboard Cables | www.2mkablo.com |


Na Juddy Ngonyani, Sumbawanga

CHAMA Cha Mapindizi (CCM), kimesema sasa kimeazimia kushirikiana na wanachama wake kuboresha maslahi ya chama hicho ikiwa ni pamoja na kuweka vitegauchumi vitakavyowaondoa wanachama hicho na dhana ya utegemezi.

Kauli hiyo ilitolewa na Katibu wa